102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
Julai/Agosti, 2010
MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA MAKADIRIO WA WILAYA YA MBOONI MAGHARIBI

Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

a. Jibu maswali manne pekee.
b. Swali la kwanza ni la **lazima.**
c. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani, Ushairi, Tamthilia, Riwaya na Fasihi simulizi.
d. Usijibu maswali **mawili** kutoka kwa kitabu kimoja.

Karatasi hii ina kurasa tano.
Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

© 2010, Mbooni West District Joint Evaluation Test

Fungua ukurasa

HADITHI FUPI

K.W Wamitila: Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi nyingine.

1. **Lazima**
Waandishi wote wa hadithi fupi za "Mayai waziri wa maradhi na hadithi nyingine".
Walikuwa na mawazo sawa katika kupitisha baadhi ya ujumbe wao. Fafanua (Alama 20)

USHAIRI

Jibu swali la 2 au la 3

2. Soma shairi hili kisha ujibu mawali yanayofuata.

Imani ya Mwana

MWANA

Kwani mamangu u ng'ombe, au u punda wa dobi?
Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi
Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi
Hebu nam bie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

MAMA

Nong'ona mwana nong'ona, sitafute angamiyo
Sinipe kuja sonona, kwa uchungu ua kiliyo
Babayo mkaii sana, kubwa pigo la babayo
Kwani kelele kunena, huyataki maishayo?
Hilo nakwambia

MWANA

Sitasakamwa kauli, nikaumiza umiyo
Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo
Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo
Baba hafanyi halali, nawe hwachi vumiliyo
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Nambie ipi sababu, yapweke kwenda kondcni
Nini yako matulubu, kulima hadi jioni?
Na jernbe ukidhurubu, ukilitua guguni
Yu wapi wako muhibu, Baba kwani simuoni?
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

© 2010, Mbooni West District Joint Evaluation Test

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?
Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mitaani
Hajali hakuthamini,wala haoni huzuni
Mwisho wa haya ni nini, ewe mama wa imani?
Hebu nambie
Kweli jaza ya. kiumbe, ni madhila na mapigo?

Na kule kondeni kwako, ukate kuni kwa shoka
Ufunge mzigo wako, utosmi kujitwika
Kwa haraka uje zako, chakula upate pika
Ukichelewa vituko, baba anakutandika
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Chakula kilicho ndani, ni jasho lako hakika
Kiishapo u mbioui, wapita kupokapoka
Urudi uje mekoni, uanze kushughulika
Ukikosa kisirani, moto nyumbani wawaka
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Na nyumbani ufagie, na nguo zake kufuwa
Wadogo uangalie, wapate kunadhifiwa
Baba umuandalie. kwa sahani na makawa
Hapo wewe ubakie, umngojee kunawa
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Na maungo umkande, umsinge kwa madawa
Mambo yasende upande, kila kitu kiwe sawa
Huoni hata ushinde, utumwa umeachiwa
Natamani nikulinde, na hii yako beluwa
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Wakati umeshafika, yapasa kujikombowa
Ukae ukikumbuka, haki zenu nyote sawa
Mpaka lini `tasumbuka, ukiteseka kwa ndowa
Na nyuma unajiweka, kwa hofu waadhibiwa
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

© 2010, Mbooni West District Joint Evaluation Test

MAMA

Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka
Ninaanza kujipinda, kwa mapambano hakika
Hilo nakwambia!

Maswali

(a) Hili ni shairi la aina gani? (Alama 2)
(b) Eleza arudhi tatu za kishairi alizotumia mshairi (Alama 3)
(c) Yaelekea mwana ananong'ona. Toa sababu (Alama 7)
(d) Andika umbo la ubeti wa pili wa mwana (Alama 4)
(e) Eleza umuhimu wa alama ya kuuliza (Alama 2)
(f) Msimamo wa mwana ni upi kuhusu anachozungumzia mshairi ? (Alama 2)

3. ***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.***

1. Tabia ni kitu,
Kuwa nayo mtu,
Akatenda utu,
Ama jambo baya,

2. Tabia siri,
Mawili hujiri,
Baya au zuri,
Moja hutokea,

3. Huwa mtu mwema,
Alo na heshima,
Na mji mzima,
SIFAYO kuenea,

4. Au kuwa na maovu,
Wa roho mbovu,
Tena mwenye wivu,
Waja kuchukia.

5. Mtu chake chanzo,
Ni la kwao funzo,
Tabia ni mwanzo,
Ya kuinukia

6. Na tabia njema,
Ni baba na mama
Wa malezi mema,
Wazazi kulea.

7. Tabia nzuri,
Ndiyo desturi,
Ni kama JOHARI,
KITO asilia.

8. Basi mwanadamu,
Kiumbe fahamu
Nawe UAZIMU,
Mja tia nia.

(a) Lipe shairi hili kichwa. (Alama 2)
(b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi. (Alama 3)
(c) Fafanua sifa bainifu za ushairi huu. (Alama 5)
(d) Dondoa na ueleze mifano miwili tofauti ya uhuru wa ushairi katika shairi hii. (Alama 4)
(e) Bali na beti, vina, mizani, na mishororo toa sifa zingine mbili kudhihirisha kuwa utunzi huu ni ushairi. (Alama 4)
(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao:
i) Alo
ii) Johari

iii) Uazimu
iv) Sifayo (Alama 2)

RIWAYA

S: A Mohamed: Utengano

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Sikutaraji kwamba mambo yatakuwa waa, kiasi hiki. Tumefuzu shoga. Pwagu limepata pwaguzi"
a. Eleza maktadha wa dondoo hili (Alama 4)
b. Wazungumzaji walifuzu kwa kufanya nini? Eleza (Alama 6)
c. Eleza madhara yaliyo sababishwa na kufaulu kwao (Alama 4)
d. Eleza sifa na umuhimu wa wanaozungumza (Alama 6)

5. "……. Mabeberu bado hatuna uhuru kamili, hatujaudhibiti uchumi, Babu we'. Usinihutubie"
a. Eleza muktadha wa maneno hayo (Alama 4)
b. "Bado hatuna uhuru" dhihirisha ukweli wa kauli hio ukirejelea riwaya ya utengano (Alama 8)
c. Eleza tabia za wahusika katika muktadha wa dondoo (Alama 8)

TAMTHILIA

Kithaka wa Mberia: Kifo Kisimani

Jibu swali la 6 au la 7

6. "Mara nyingi vijana hushughulika mambo ya kibinafsi. Mara nyingi mawazo yao hufuata mkondo wa anasa za vijana tu"
a. Onyesha ushahidi wowote katika tamthilia kudhihirisha ukweli wa kauli hii (Alama 8)
b. Fafanua mambo waliyoyafanya vijana katika Jamii ya kifo kisimani kuonyesha walipigana kwa niaba ya umma (Alama 12)

FASIHI SIMULIZI

7. a. Eleza maana ya kitendawili. (Alama 2)
b. Taja sifa sita za vitendawili. (Alama 6)
c. Taja na ueleze aina tatu za vitendawili. (Alama 6)

© 2010, Mbooni West District Joint Evaluation Test